Washington State
Department of Social & Health Services

# ILANI YA KAZI ZA FARAGHA
# KWA HABARI ZA SIRI ZA MTEJA
## NOTICE OF PRIVACY PRACTICES FOR CLIENT CONFIDENTIAL INFORMATION
## Kuanzia Aprili 14, 2003

Sheria inahitaji DSHS ikuarifu juu ya haki zako za siri. Ilani hii haiathiri kustahiki kwako huduma za DSHS.

**Ilani hii inafafanua jinsi habari za kitabibu na zingine za siri kukuhusu wewe zinaweza kutumiwa na kufichuliwa na jinsi unavyoweza kuona habari hizi. Tafadhali ihakiki kwa makini.**

**Je, ni habari zipi za siri ambazo DSHS inazo kunihusu?**

Unawezakuwa unaomba, au kuhusika katika mipango ya DSHS ambayo inatoa faida au huduma. Kama sehemu ya utaratibu huo, unaweza kuhitajika kutoa habari za siri kama vile habari za mawasiliano, kifedha, na za kiafya. Tunaweza pia kupokea habari za siri kukuhusu kutoka kwa vyanzo vingine ambavyo tunahitaji ndipo tuweze kukuhudumia au kutoa malipo kwa huduma yako.

**Je, ni nani anayeona habari zangu za siri?**

Tunaona kiwango cha chini tu cha habari za siri ambazo tunahitaji ili kufanya kazi zetu. Tunaweza kushiriki habari na mipango au watu wengine kama inaruhusiwa na sheria au na wewe. Kwa mfano, habari za siri kuhusu afya yako zinaweza kutolewa na kutumiwa na watoa huduma ya afya ambao wanakuhudumia. Tunaweza kushiriki habari za zamani, za sasa au za usoni.

**Je, ni habari zipi ambazo DSHS hushiriki?**

Tunashiriki habari kukuhusu wewe tu ambazo zinahitajika na wengine ili wafanye kazi zao. Unaweza kuuliza orodha ya sehemu ambazo tumetuma habari zako za afya.

**Je, ni lini DSHS hushiriki habari za siri?**

Tunaweka na kushiriki habari ili kuratibisha matibabu, malipo na utendaji kazi wa chombo. Tunaweza kushiriki habari ili:

- Kuamua kama matibabu yanafaa.
- Kulipa huduma kutoka kwa watoa huduma za afya.
- Kuamua kustahiki kwako huduma na faida.
- Kutathmini ubora wa huduma unayopokewa kutoka kwa watoa huduma.

**Ninaweza kuona habari zangu?**

Unaweza kuona habari ambazo tunazo kukuhusu. Kama una rekodi kwa zaidi ya sehemu moja ya DSHS, unastahili kutuambia ni rekodi zipi unazotaka kuona. Ukiomba, utapokea nakala. DSHS inaweza kukulipisha kwa nakala za rekodi zako.

**Ninaweza kubadilisha rekodi zangu?**

Kama unadhania habari za afya katika rekodi yako si sahihi, unaweza kutuma ombi lililoandikwa kwamba turekebishe au tuongeze habari mpya. Unaweza pia kuuliza kwamba tutume marekebisho kwa wengine ambao wamepokea nakala za rekodi zako.

**Na je kama mtu mwingine anahitaji habari zangu za siri?**

Unaweza kuulizwa uweke saini fomu ya kuidhinisha ukiruhusu habari zako zishirikiwe kama:

- DSHS inahitaji kutuma habari kwa sehemu zingine;
- Unataka sisi tutume habari kwa chombo au mtoa huduma mwingine;
- Unataka habari zitumwe kwa mtu mwingine kama vile wakili, jamaa au mwakili wako mwingine.

Idhini yako ya kushiriki habari zako inatumika hadi tarehe uliyowekwa kwenye fomu ya kuidhinisha. Tunaweza kushiriki habari ambazo umeorodhesha tu. Unaweza kuondoa au kubadilisha idhini hii kwa kuandika.

**ILANI YA DSHS YA KAZI YA FARAGHA KWA HABARI ZA SIRI**
**Kuanzia Aprili 14, 2003**

**Je, habari za siri zinaweza kushirikiwa bila idhini yangu?**

Ndiyo, kuna wakati ambao habari za siri zinaweza kushirikiwa bila idhini yako. Kisheria, wakati mwingine tunahitajika au kuruhusiwa kushiriki habari za siri kukuhusu, hata kama hujatupa idhini. Baadhi ya hali hizi ni:

- Kuripoti matukio ya mtoto au mtu mzima kudhulumiwa au polisi au vyombo vingine vinavyofaa kupuuza;
- Kutoa rekodi unapoamrishwa kufanya hivyo na korti;
- Kutoa habari kwa vyombo vingine ambavyo vinahakiki kazi za DSHS;
- Kushiriki habari na vyombo vya serikali ambavyo vinatoa leseni na kukagua vifaa vya matibabu, kama vile vyumba vya wagonjwa na hospitali;
- Kushiriki habari zinazohitajika na watoa huduma au vyombo vingine ili kuamua kama unastahiki huduma au faida;
- Kutoa habari zingine kwa wazazi au walezi wa watoto;
- Kutumia habari kwa madhumuni ya utafiti.

**Ninaweza kuweka vizuizi kwa kushiriki habari zangu na jinsi ninavyozipokea?**

Unaweza kutuuliza tuzuie utumiaji na utoaji wa habari zako za afya lakini sio lazima tukubali. Unaweza pia kuuliza kwamba tutume habari hizi kwako kwa fomati tofauti au kwa eneo tofauti.

**Ninaweza kupata nakala ya ilani hii?**

Ndiyo. Ilani hii ni yako ya kutunza. Ikiwa ulipokea ilani hii kielektroniki, unaweza kuuliza nakala ya karatasi na tutakupa moja.

**Na je kazi za faragha zikibadilika?**

Tuna haki ya kubadilisha kazi katika ilani hii. Sheria ikibadilika, tutakutumia ilani mpya kuhusu mabadiliko hayo.

**Niwasiliane na nani kama nina maswali kuhusu ilani hii au haki zangu?**

Ikiwa una maswali yoyote kuhusu ilani hii, tafadhali uliza mtu aliyekupa. Ikiwa unahitaji msaada zaidi, unaweza kumpigia simu Afisa wa Faragha wa DSHS nambari ya simu (360) 902-8278.

**Ninawezaje kuripoti ukiukaji wa haki za siri?**

Ikiwa unaamini haki zako za siri zimevunjwa unaweza kuwasilisha malalamiko kwa:

Afisa wa DSHS Privacy Officer, Department of Social and Health Services, PO Box 45115, Olympia WA 98504-5115. Ukiwasilisha malalamiko, DSHS haitabadilisha au kusimamisha huduma au faida zako na haiwezi kulipiza kizazi kinyume chako.

**AU**

Katibu, Secretary, Department of Health and Human Services (DHHS), 2000 Independence Avenue, Washington, D.C. 20201. Malalamiko yoyote lazima yawasilishwe kwa DHHS kati ya siku180 za ukiukaji siri.

Washington State Department of Social & Health Services

**ILANI YA DSHS YA KAZI ZA FARAGHA KWA HABARI ZA SIRI**
**Kuanzia Aprili 14, 2003**

# KUKUBALI

## ACKNOWLEDGEMENT

| JINA LA MTEJA (TAFADHALI ANDIKA) | TAREHE YA MTEJA KUZALIWA |
|---|---|
| | |

**Nimepokea nakala ya Ilani ya Siri ya DSHS na nimekua na nafasi ya kuuliza maswali kuhusu jinsi habari zangu za siri za afya zitatumiwa na kushirikiwa na DSHS.**

| SAINI YA MTEJA AU MWAKILISHI WA KIBNAFSI | TAREHE |
|---|---|
| | |

**FOR DSHS USE ONLY (KWA MATUMIZI YA DSHS TU)**

**To be completed if unable to obtain client’s or personal representative’s signature.**

Describe efforts made to have the client acknowledge receipt of the Notice of Privacy Practices (NPP):

Describe reason why acknowledgement was not obtained:

| STAFF MEMBER’S NAME AND TITLE (PLEASE PRINT) | ADMINISTRATION/DIVISION |
|---|---|
| | |

| STAFF’S SIGNATURE | DATE |
|---|---|
| | |